Core Humanitarian
STANDARD

# Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kuhusu Ubora na Uwajibikaji

**Kimechapishwa na:** CHS Alliance, Groupe URD na Mradi wa Sphere.

**Toleo la kwanza:** 2014

**ISBN: 978-0-9955053-1-5**

© Haki zote zimehifadhiwa. Hakimiliki ya maudhui yaliyomo hapa ni ya CHS Alliance, Groupe URD na Mradi wa Sphere. Maudhui haya yanaweza kuchapishwa upya kwa madhumuni ya kielimu, ikiwa ni pamoja na mafundisho, utafiti na shughuli za miradi, maadamu Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kinachohusu Ubora na Uwajibikaji kimefuatwa. Ili kutafsiri au kuomba sehemu ndogo au maudhui yote ya Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kinachohusu Ubora na Uwajibikaji, ni sharti mhusika apewe ruhusa kwa kutuma barua pepe kwa info@corehumanitarianstandard.org.

# Dibaji

Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kinachohusu Ubora na Uwajibikaji (CHS) kinatokana moja kwa moja na Mpango wa Viwango Shirikishi (JSI) ambapo Ushirikiano wa Uwajibikaji wa Kibinadamu (HAP) Kimataifa, shirika la Watu wanaotoa Misaada na Mradi wa Sphere ziliungana ili kutafuta mshikamano mkubwa zaidi wa watumiaji wa viwango vya kibinadamu. JSI ilishauriana na wahudumu zaidi ya 2000 wa kibinadamu katika afisi kuu, maeneo na mataifa yanayokumbwa na mikasa mara kwa mara. Maoni waliopata yaliangazia haja ya kuoanisha viwango, huku jamii na watu walioathiriwa wakipewa kipaumbele na kanuni za kibinadamu zikiwa msingi wa viwango hivi.

CHS imetokana na ushauriano wa miezi 12 na awamu tatu, ambapo wahudumu wa kibinadamu, jamii na watu walioathiriwa na mikasa, mamia ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na mitandao, serikali, Umoja wa Mataifa na wakala wa ufadhili na wasomi walichanganua maudhui ya CHS kwa kina na kuyatathmini katika kiwango cha makao makuu na nyanjani.

Maoni yaliyokusanywa kwenye kila ushauri yalichambuliwa na marekebisho yake kuidhinishwa na Kundi la Kiushauri wa Kiufundi la watu 65 lililowakilisha maeneo mengi wakilishi ya utaalam wa kiufundi katika utendaji wa kibinadamu na ukuzaji viwango.

Bodi za HAP International, Watu wanaotoa Misaada na Mradi wa Sphere zinatarajia kwamba CHS itachukua nafasi ya Usimamizi wa Kiwango cha 2010 cha HAP cha Uwajibikaji na Ubora, Kanuni ya Maadili Bora ya Watu wanaotoa Misaada katika Usimamizi na Usaidizi wa Wahudumu wa Usaidizi na sehemu ya viwango vikuu katika Mwongozo wa Sphere.

# Shukrani


Tunazishukuru mamia ya mashirika na watu binafsi walioshiriki katika uandalizi wa CHS na kutoa maoni kuhusu rasimu za CHS, kwa kuzifanyia majaribio katika mashirika yao, au kwa kushiriki katika mojawapo ya vikundi vilivyowezesha shughuli ya ushauri ya CHS[1], au kwa kushiriki katika mojawapo ya vikundi vilivyowezesha shughuli ya ushauri ya CHS. Tulifurahishwa na kuhusika kwa jamii mbalimbali na watu walioathiriwa na mikasa katika mchakato wa ushauri na utathmini.

Groupe URD iliungana na HAP International, Watu wanaotoa Misaada na Mradi wa Sphere katika kujumuisha mfumo wa urejeleaji wa DIRA ya Ubora katika CHS. Kikundi cha CHS cha Ushauri wa Kiufundi na kikundi chake tanzu cha Kamati Elekezi ya Kiufundi ni vikundi vilivyowajibikia mchakato wa ushauri na uidhinishaji hatima wa CHS. Kikundi cha Uandishi cha CHS kilipewa jukumu la kurekebisha CHS kwa kujumuisha maoni yaliyopokelewa katika kila awamu ya ushauri.


[1] Orodha kamili ya mashirika yaliyofanya majaribio ya CHS yanapatikana kwenye www.corehumanitarianstandard.org.

Ili kuhakikisha kwamba matokeo ya mwisho yalikuwa jumuishi, wakilishi na ya kikweli, mchakato wa ushauri wa CHS uliongozwa na WolfGroup Consultants kwa njia huru.

Orodha kamili ya wanachama wa Kikundi cha Ushauri wa Kiufundi, Kikundi Elekezi cha Kiufundi na Kikundi cha Uandishi inaweza kupatikana katika www.corehumanitarianstandard.org. Ushauri wa CHS haungewezekana bila usaidizi wao mkubwa.

Mchakato wa Kiwango Kikuu cha Kibinadamu ulifadhiliwa pakubwa na wafadhili wafuatao: Idara ya Serikali ya Australia ya Masuala ya Kigeni na Biashara; Wakala wa Kikatoliki wa Maendeleo ya Ng'ambo (CAFOD); Wizara ya Masuala ya Kigeni ya Denmaki (Danida); Afisi ya Kigeni ya Jamhuri ya Kishirikisho ya Ujerumani; Irish Aid; Wakala wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa wa Uswidi; Wakala wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa wa Uswizi; UK Aid kutoka Serikali ya Uingereza; na Serikali ya Marekani.

HAP International, Watu wanaotoa Misaada na Mradi wa Sphere pia wangependa kuwashukuru wanachama wafuatao wa bodi kwa mchango wao wa kifedha kwa ajili ya mchakato wa CHS. ACT Alliance; ActionAid International; Aktion Deutschland Hilft; Shirika la Msalaba Mwekundu la Uingereza; Wakala wa Kikatoliki wa Maendeleo ya Ng'ambo (CAFOD); CARE International; Christian Aid; Community World Service Asia; DanChurchAid; Shirikisho la Dunia la Kilutherani; Save the Children International; Save the Children US; na World Vision International.

## Maoni

Tungependa kupokea maoni kuhusu CHS wakati wowote, na yanaweza kutumwa, pamoja na maswali, kupitia info@corehumanitarianstandard.org.

## Ukaguzi

Maoni yote yaliyopokelewa yatashughulikiwa katika marekebisho ya CHS, ambayo yatafanywa kabla ya mwisho wa Disemba 2019. Tembelea www.corehumanitarianstandard.org upate maelezo zaidi kuhusu Kiwango Kikuu cha Kibinadamu, nyenzo husika na hati nyingine zinazoendelea kuandaliwa.

## Kidokezo kuhusu tafsiri

Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kitatafsiriwa kwa Kiarabu, Kifaransa na Kihispania. Ikiwa ungependa kutafsiri CHS kwalugha nyingine, tafadhali wasiliana na info@corehumanitarianstandard.org upate ushauri wa kutafsiri. Tafsiri zote zitapatikana bila malipo kupitia tovuti ya www.corehumanitarianstandard.org.

## Nyenzo husika

Ushauri na zana za kuwezesha utekelezaji wa CHS zinapatikana bila malipo kwenye tovuti ya www.corehumanitarianstandard.org.

# Orodha ya Yaliyomo


i. Utangulizi 2 - 3

ii. Muundo wa Kiwango Kikuu cha Kibinadamu (CHS) 5

iii. Kutekeleza CHS 6 - 7

iv. Madai 7

v. Usaidizi wa Kibinadamu Unaofuata Kanuni 8

vi. Maazimio Tisa na ubora Utaratibu 9

vii. Maazimio, Hatua na Majukumu 10 - 18

1. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapokea usaidizi unaoambatana na mahitaji yao. 10
2. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wana uwezo wa kufikia usaidizi wa kibinadamu wanaohitaji kwa wakati unaofaa. 11
3. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa hawajapata madhara na wamejitayarisha, wako imara na hawako katika hatari kubwa kutokana na hali ya kibinadamu. 12
4. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanajua haki zao, wanafikia habari na wanahusika katika uamuzi unaowahusu. 13
5. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wana uwezo wa kufikia taratibu salama na bora za kushughulikia malalamishi. 14
6. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapata usaidizi ulioratibiwa na wa kukamilishana. 15
7. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanaweza kutarajia kupata usaidizi bora mashirika yanavyojifunza kutoka kwa mambo ya awali na mawazo. 16
8. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapata usaidizi wanaohitaji kutoka kwa wahudumu waajiriwa na wa kujitolea wenye ustadi na wanaosimamiwa vizuri. 17
9. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanaweza kutarajia kuwa mashirika yanayowasaidia yanatumia raslimali vizuri na kiuadilifu. 18

viii. Faharasa 19

# Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kuhusu Ubora na Uwajibikaji

## i. Utangulizi

Kila kukicha kote duniani, idadi kubwa ya watu kutoka matabaka mbali mbali huchukua hatua muhimu za kibinadamu - hamu ya kuzuia na kupunguza mateso kwa binadamu janga zinapotokea.

Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kinachohusu Ubora na Uwajibikaji (CHS) kimeweka Maazimio Tisa ambayo mashirika na watu binafsi wanaohusika katika usaidizi wa kibinadamu wanaweza kutumia kuboresha na kunufaisha usaidizi wanaotoa. CHS pia huwezesha uwajibikaji zaidi kwa jamii na watu walioathiriwa na mikasa: kufahamu maazimio ya mashirika kutawasaidia kuyashinikiza yawajibike.

CHS huzipa kipaumbele jamii na watu walioathiriwa na mikasa katika usaidizi wa kibinadamu na kuhimiza kuheshimu haki zao za kibinadamu.

CHS imeungwa mkono na haki ya uhai ulio na hadhi, na haki ya ulinzi na usalama kama ilivyoainishwa katika sheria za kimataifa, ikijumuisha Mswada wa Kimataifa wa Haki za Kibinadamu.[2]

Kama kiwango kikuu, CHS inaeleza vipengele muhimu vya shughuli thabiti, zenye kuwajibika na bora za kibinadamu. Mashirika ya kibinadamu yanaweza kuitumia kama kanuni ya hiari ya kuratibisha taratibu zao za ndani. CHS pia inaweza kutumiwa kama msingi wa kuthibitisha utendaji, ambapo mfumo maalum na viashiria husika vimewekwa ili kuhakikisha ufaafu wake katika miktadha na aina mbalimbali za usimamizi wa mashirika.


[2] Mswada wa Kimataifa wa Haki za Kibinadamu unajumuisha Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Kiuchumi, Haki za Kijamii na Kitamaduni na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Umma na Kisiasa na Itifaki zake za Hiari.

CHS inaweza kukuzwa na kutekelewa na watu binafsi, mashirika, taasisi za uratibu, ubia na vikundi vingine vinavyohusika au kuchangia katika usaidizi wa kibinadamu. Ingawa CHS imekusudiwa kimsingi kutumika katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu, pia inaweza kutumika na shirika lolote kuimarisha ubora wa juu na uwajibikaji mkubwa katika vipengee vyote vya kazi yake katika jamii na watu walioathiriwa na mikasa.

CHS ni matokeo ya mchakato wa mashauriano ya kimataifa. CHS huunganisha vipengee vikuu vya maazimio na viwango vilivyopo vya kibinadamu. Viwango hivi vinajumuisha vifuatavyo, na vinginevyo:

- Kanuni ya Maadili ya Shirika la Msalaba Mwekundu la Kimataifa na Vuguvugu la Hilali Nyekundu na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayohusika katika Usaidizi wakati wa Majanga;
- Kiwango cha 2010 cha HAP katika Uwajibikaji na Usimamizi wa Ubora;
- Kanuni ya Maadili Bora ya Watu wanaotoa Misaada katika Usimamizi na Usaidizi wa Wahudumu wa Kimsaada;
- Viwango Vikuu vya Mwongozo wa Sphere na Mkataba wa Kibinadamu;
- DIRA ya Ubora;
- Kamati ya Kudumu ya Wakala Nyingi ya Uwajibikaji kwa Jamii na Watu Walioathiriwa (CAAPs); na
- Utaratibu wa Kutathmini Maendeleo na Usaidizi wa Kibinadamu wa Kamati ya Usaidizi wa Kimaendeleo (DAC) ya Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD).

## Muundo wa Kiwango Kikuu cha Kibinadamu kinachohusu Ubora na Uwajibikaji



# ii. Muundo wa Kiwango Kikuu cha Kibinadamu

CHS ni mkusanyiko wa Maazimio Tisa kwa jamii na watu walioathiriwa na mikasa, yanayoainisha matarajio yao kutoka kwa mashirika na watu binafsi katika utoaji usaidizi wa kibinadamu. Kila Azimio linaungwa mkono na Utaratibu wa Ubora unaoeleza jinsi mashirika ya usaidizi wa kibinadamu na wahudumu wake wanavyopaswa kufanya kazi ili kuuttimiza utaritibu huu. CHS ina muundo ufuatao:

- Maazimio Tisa;
- Taratibu saidizi za Ubora;
- Hatua Muhimu zitakazochukuliwa ili kutimiza Maazimio; na
- Majukumu ya Kishirika ili kuunga mkono utekelezaji dhabiti na unaofuata taratibu maalum wa Hatua Muhimu katika shirika lote.

Hatua Muhimu na Majukumu ya Kishirika mtawalia hueleza kuhusu:

- hatua ambazo wahudumu wa usaidizi wa kibinadamu wanapaswa kuchukua ili kutekeleza mipango ya ubora wa juu kwa njia thabiti na wawajibikie watu wanaowasaidia; na
- sera, taratibu na mifumo ambayo mashirika yanayohusika katika usaidizi wa kibinadamu yanapaswa kutekeleza ili kuhakikisha kwamba wahudumu wao wanatoa usaidizi wa ubora wa juu na wenye uwajibikaji.

Faharasa ya maneno yanayotumika katika CHS yenye ufasili maalum yamejumuishwa mwishoni mwa hati hii.

# iii. Kutekeleza CHS

Mashirika yanayojitoa kufuata CHS yanalenga kutimiza Maazimio yote Tisa. Matarajio ya chini zaidi ni kwamba yanapaswa kutia juhudi kila mara ili kuboresha mifumo, miundo na mbinu zao ili kuimarisha ubora na uwajibikaji wa usaidizi wao wa kibinadamu kila mara.Hata hivyo, mashirika na watu binafsi wanaohusika katika usaidizi wa kibinadamu ni wa aina mbalimbali. Wanahitaji kuchukua hatua wakati ufaao na kubadilisha mbinu zao kulingana na uwezo na majukumu ya mashirika yao, na pia awamu na hali ya mikasa wanayokabiliana nayo.

Mashirika yakikabiliwa na changamoto katika kutimiza Maazimio Tisa, wanapaswa kukubali hali hii na kubaini jinsi ya kushughulikia masuala yanayowakabili. Mashirika yanapaswa kujifunza kutokana na hali kama hizi, na kuanzisha mbinu za kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

Uchanganuzi wowote wa utekelezaji CHS unapaswa kuwekwa kwenye msingi wa kiwango cha utendakazi wa shirika lolote katika kutimiza Maazimio Tisa wala si kwa msingi wa kutekeleza Hatua Muhimu na/au Majukumu ya Kishirika tu. Kwa hivyo, hatua Muhimu zinazohitajika na CHS zinahitaji kubadilishwa ili zifae muktadha husika.

CHS hutumika kwa mashirika na watu binafsi ambao:

- hutoa usaidizi wa moja kwa moja kwa jamii na watu walioathiriwa na mikasa hupokea;
- hutoa usaidizi wa kifedha, nyenzo na kiufundi kwa mashirika mengine, lakini hawahusiki moja kwa moja katika kutoa usaidizi; au
- huunganisha mbinu hizi mbili.

CHS imeundwa ili itumike kwa njia kadhaa na watu wanaohusika katika usaidizi wa kibinadamu, ikijumuisha njia ya:

- kuwezesha uwajibikaji zaidi kwa jamii na watu walioathiriwa na mikasa, na kuimarisha ubora wa huduma wanazopokea;
- kuandaa mipango ya utendakazi kwa ajili ya utekelezaji endelevu na uboreshaji endelevu wa CHS;
- kufuatilia ubora na uwajibikaji, kwa kutumia mfumo wa CHS ili kuunga mkono viwango vilivyopo vya kishirika na kiufundi;
- kutathmini kibinafsi na kuimarisha ubora wa mipango;
- kuthibitisha au kuidhinisha maafikiano, na kuonyesha maafikiano haya kwa wengine; na
- kutathmini, ikiwa ni muhimu, umbali ambao michakato na usaidizi wa ndani unatimiza usaidizi na majukumu ya kishirika kama yaliyowekwa katika CHS.

Inabidi mashirika yanayoamua kutumia CHS kuikuza ndani na nje ya shirika.

Inabidi mashirika yanayo hudumu kupitia mashirika mengine kueleza dhamira kwa CHS na kuhakikisha uelewa[3] zingatia maazimio tisa na kuhakikisha mbinu ya kutekeleza maazimio ya CHS.

## iv. Madai

Mtu binafsi au shirika lolote linalohusika katika usaidizi wa kibinadamu linahimizwa kutumia na kufuata CHS na linaweza kusema: "tunaendelea kutia juhudi za kutekeleza CHS." Mashirika yanaweza kudai kwamba yanazingatia CHS ikiwa yamefanya uthibitisho halisi kwa kujilinganisha na CHS yenyewe.

[3] Tazama fasili katika faharasa.

# v. Usaidizi wa Kibinadamu Unaofuata Kanuni

Watu ndio lengo kuu katika usaidizi wa kibinadamu. Kichocheo kikuu cha usaidizi wowote katika mikasa ni kuokoa maisha, kupunguza mateso ya kibinadamu na kuunga mkono haki ya kuishi kwa hadhi.

Mashirika ya usaidizi wa kibinadamu yanatambua kwamba umuhimu wa maisha ya binadamu hupewa kipaumbele, na hivyo hulenga kutoa usaidizi wa kibinadamu popote unapohitajika.

Usaidizi wa kibinadamu huongozwa na kanuni nne zinazokubalika na watu wengi[4]:

- Ubinadamu: Mateso ya binadamu yanapaswa kushughulikiwa popote yanapopatikana. Madhumuni ya usaidizi wa kibinadamu ni kulinda maisha na afya, na kuhakikisha kwamba binadamu wameheshimiwa.
- Kutobagua: Usaidizi wa kibinadamu ni sharti utekelezwe kwa msingi wa mahitaji pekee, huku matukio ya dharura ya mikasa yakipewa kipaumbele na kutowabagua watu kwa msingi wa utaifa, rangi, jinsia, imani ya kidini, hadhi au msimamo wa kisiasa.
- Uhuru: Usaidizi wa kibinadamu ni sharti uwe huru kutokana na malengo ya kisiasa, kiuchumi, kijeshi na mengineyo, ambayo mshiriki yeyote huenda awe nayo dhidi ya maeneo ambapo usaidizi wa kibinadamu unatekelezwa.
- Kutoegemea upande wowote: Washiriki wa usaidizi wa kibinadamu ni sharti wasiegemee upande wowote katika uhasama wala wasihusike katika mabishano ya kisiasa, rangi, dini au dhana.[5]

Kanuni za kibinadamu ziko katika msingi wa kazi yote ya usaidizi wa kibinadamu.Zinaongoza usaidizi wa kibinadamu na jinsi ya kuyatimiza na kutofautisha kati ya shughuli za kibinadamu na shughuli zinginezo. Katika CHS, kanuni nne za kibinadamu zimeratibishwa kwenye maazimio, ubora utaratibu, hatua muhimu na majukumu ya kishirika.

Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, Sheria ya Kimataifa ya Haki za Kibinadamu na Sheria ya Kimataifa ya Wakimbizi iliweka viwango muhimu vya kisheria zinazohusiana na ulinzi wa vikundi na watu binafsi, na pia kuhusiana na aina ya usaidizi ambao unafaa kutolewa kwao. Mkataba wa Kibinadamu wa Sphere unatoa muhtasari wa kanuni kuu za kisheria zilizo muhimu zaidi kwa maslahi ya watu walioathiriwa na mikasa au mzozo.

Watu wanaotekeleza Kiwango Kikuu cha Kibinadamu wanatambua jukumu kuu la mataifa na mamlaka nyingine husika katika kulinda na kuwasaidia watu walioathiriwa na mikasa au mizozo ya kivita katika maeneo yao. Usaidizi wa kibinadamu unastahili kuendeleza majukumu haya badala ya kuyadhoofisha.

[4] Kanuni Kuu za Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu na Vuguvugu la Hilali Nyekundu zilizotangazwa jijini Vienna mwaka wa 1965 katika Kongamano la 20 la Kimataifa la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu; Azimio la 46/182 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, tarehe 19 Desemba 1991; na Azimio la 58/114 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, tarehe 5 Februari 2004.

[5] Licha ya kuapa kutoa usaidizi bila ubaguzi na kutoegemea upande wowote katika uhasama, baadhi ya mashirika hayazingatii kwamba kanuni ya kutoegemea upande wowote huwazuia kutetea masuala yanayohusu haki na uwajibikaji.

# vi. Maazimio Tisa na ubora Utaratibu

**1. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapokea usaidizi unaoambatana na mahitaji yao.**
**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu ni mwafaka na muhimu.

**2. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wana uwezo wa kufikia usaidizi wa kibinadamu wanaohitaji kwa wakati unaofaa.**
**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu una ufanisi na hufanywa wakati unaofaa.

**3. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa hawajapata madhara na wamejitayarisha, wako imara na hawako katika hatari kubwa kutokana na hali ya kibinadamu.**
**Kigezo cha Ubora:** Utaratibu wa Ubora: Usaidizi wa kibinadamu huimarisha uwezo wa mahali palipoathiriwa na kuepuka madhara.

**4. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanajua haki zao, wanafikia habari na wanahusika katika uamuzi unaowahusu.**
**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu huwekwa katika msingi wa mawasiliano, ushiriki na kutoa maoni.

**5. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wana uwezo wa kufikia taratibu salama na bora za kushughulikia malalamishi.**
**Kigezo cha Ubora:** Malalamiko hupokewa na kushughulikiwa.

**6. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapata usaidizi ulioratibiwa na wa kukamilishana.**
**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu hufanywa kwa uratibu na humarisha hali zilizopo.

**7. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanaweza kutarajia kupata usaidizi bora mashirika yanavyojifunza kutoka kwa mambo ya awali na mawazo.**
**Kigezo cha Ubora:** Wasaidizi wa kibinadamu hupata maarifa na kuyaboresha kila mara.

**8. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapata usaidizi wanaohitaji kutoka kwa wahudumu waajiriwa na wa kujitolea wenye ustadi na wanaosimamiwa vizuri.**
**Kigezo cha Ubora:** Wahudumu wanasaidiwa kufanya kazi zao ifaavyo, na wanashughulikiwa vizuri na kwa usawa.

**9. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanaweza kutarajia kuwa mashirika yanayowasaidia yanatumia raslimali vizuri na kiuadilifu**
**Kigezo cha Ubora:** Raslimali zinasimamiwa na kutumiwa kiuadilifu kwa malengo yaliyokusudiwa.

# vii. Maazimio, Hatua na Majukumu

## 1. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapokea usaidizi unaoambatana na mahitaji yao.

**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu ni mwafaka na muhimu.

**Shughuli Kuu**

**1.1** Kutekeleza uchangunuzi wa taratibu, usio na upendeleo na unaoendelea wa kimuktadha na washika dau.

**1.2** Kubuni na kutekelezamipango bora kulingana na utathmini usio na upendeleowa mahitaji[6] na hatari, na kuelewa hatari na uwezo wa makundi tofauti[7].

**1.3** Kulinganisha programu kwa mahitaji, uwezo na muktadha unaobadilika.

**Wajibu wa Shirika**

**1.4** Sera zinanuiwa kutoa usaidizi usio na upendeleo kulingana na mahitaji na uwezo wa jamii na watu walioathiriwa na mikasa.

**1.5** Sera zinatoa maazimio yanayozingatia tofauti za jamii, wakiwemo watu waliotengwa au kubaguliwa, na kuchukua data ambayo haijakusanywa.

**1.6** Mbinu zimeundwa kuhakikisha kuwa uchanganuzi bora na endelevu wa muktadha.

[6] "Mahitaji" yanashirikisha usaidizi na kinga.
[7] Hii inaweza kumaanisha, kwa mfano: wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, vijana, na wazee, vile vile watu walio na ulemavu na makabila maalum madogo bila ubaguzi wowote.

## 2. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wana uwezo wa kufikia usaidizi wa kibinadamu wanaohitaji kwa wakati unaofaa.

**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu una ufanisi na hufanywa wakati unaofaa.

**Shughuli Kuu**

**2.1** Buni mipango inayoshughulikia ugumu[8] ili shughuli iliyopendekezwa iweze kutimikana iwe salama kwa jamii.

**2.2** Toa usaidizi wa kibinadamu kwa wakati mwafaka, ukifanya uamuzi na kutoa usaidi bila kuchelewa.

**2.3** Peleka mahitaji yoyote yasiyotimika kwa mashirika yaliyo na ujuzi mwafaka wa kiufundi, au ushinikize utatuaji wa mahitaji hayo.

**2.4** Tumia viwango mwafaka vya kiutendaji na utendaji bora unaotumika kote katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu ili kupanga na kutathmini mpango.

**2.5** Fuatilia shughuli, mazao na matokeo ya usaidizi wa kibinadamu ili kulinganisha mipango na kutatua utendakazi duni.

**Wajibu wa Shirika**

**2.6** Maazimio ya mipango yanalingana na uwezo wa shirika.

**2.7** Maazimio ya kisera huhakikisha:
a. ufuatiliaji na utathmini taratibu, usio na upendeleo na endelevu wa shughuli na athari;
b. ushahidi kutoka kwa ufuatiliaji na utathmini unatumika kulinganisha na kuboresha programu; na
c. uamuzi wa haraka na utoaji bora wa raslimali.

[8] Kwa mfano, ufikiaji wa kibinadamu, usalama, utaratibu wa ugavi na usafirishaji, na ufadhili.

## 3. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa hawajapata madhara na wamejitayarisha, wako imara na hawako katika hatari kubwa kutokana na hali ya kibinadamu.

**Kigezo cha Ubora:** Utaratibu wa Ubora: Usaidizi wa kibinadamu huimarisha uwezo wa mahali palipoathiriwa na kuepuka madhara.

**Shughuli Kuu**

**3.1** Hakikisha mipango imeandaliwakulingana nauwezo wa mahali palipoathiriwa na inatekeleza wajibu wa kuboresha uthabiti wa jamii na watu walioathiriwa na mikasa.

**3.2** Tumia matokeo ya utathmini uliopo wa athari kwa jamii na mipango ya utayari ili kuelekeza shughuli.

**3.3** Wezesha uimarikaji wa uongozi na mashirika ya mahali palipoathiriwa katika uwezo wao kama wasaidizi wa kwanza katika mikasa ya baadaye, ukichukua hatua kuhakikisha kuwa makundi yaliyotengwa yamewakilishwa kikamilifu.

**3.4** Panga mkakati wa mageuzi au kuondoka katika hatua za mapema za programu hiyo ya kibinadamu unaohakikisha athari bora za muda mrefu na kupunguza hatari ya utegemezi.

**3.5** Buni na utekeleze programu zinazoendeleza ukabilianaji wa mapema wa mikasa na kufaidi uchumi wa mahali palipoathiriwa.

**3.6** Tambua na ushughulikie athari mbaya zilizopo au zinazotarajiwa kwa wakati mwafaka na kwa utaratibu, zikiwemo:
a. usalama, heshima na haki za watu;
b. unyanyasaji wa kingono na kutumiwa vibaya kwawahudumu;
c. uhusiano wa kitamaduni, kijinsia, na kijamii na kisiasa;
d. riziki;
e. uchumi wa mahali palipoathiriwa; na
f. mazingira.

**Wajibu wa Shirika**

**3.7** Sera, Mikakati na miongozo imebuniwa:
a. Kuzuia programu kuwa na athari zozote mbaya, kama vile, unyanyasaji, au ubaguzi na wahudumu dhidi ya jamii na watu walioathiriwa na mikasa; na
b. kuimarisha uwezo wa mahali palipoathiriwa.

**3.8** Taratibu zimewekwa kulinda maelezo yoyote ya kibinafsi yanayotolewa kwa jamii na watu walioathiriwa na mikasa yanayoweza kuwaweka katika hatari.

## 4. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanajua haki zao, wanafikia habari na wanahusika katika uamuzi unaowahusu.

**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu huwekwa katika msingi wa mawasiliano, ushiriki na kutoa maoni.

**Shughuli Kuu**

**4.1** Toa habarikwa jamii na watu walioathiriwa na mikasa kuhusu shirika lako, kanuni linazozingatia, matarajio yake kwawahudumu wake, mipango linayotekeleza na wanayotarajia kuafikia.

**4.2** Wasiliana kwa lugha, njia, na mbinu zinazoeleweka kwa urahisi, zenye heshima na zinazokubalika kitamaduni kwa wanajamii tofauti, hasa wanyonge na waliobaguliwa.

**4.3** Hakikisha uwakilishaji ni wa kijumla, unaohusisha ushiriki na uhusikaji wa jamii na watu walioathiriwa na mikasa katika hatua zote za kazi hiyo.

**4.4** Himiza na uwezeshe jamii na watu walioathiriwa na mikasa kutoa maonikuhusu kiwango chao cha kuridhika na ubora na ufaafu wa usaidizi waliopokea, ukizingatia hasa jinsia, umri na utofauti wa wanaotoa maoni.

**Wajibu wa Shirika**

**4.5** Sera ya usambazaji habari zipo, na zinaendeleza mawasiliano wazi.

**4.6** Sera zipo za kuhusisha jamii na watu walioathiriwa na mikasa, kuwazia umuhimu na hatari wanazotambua katika hatua zote za kazi.

**4.7** Mawasiliano ya nje, yakiwemo yanayotumika kutafuta ufadhili ni kamilifu, ya kimaadili, yenye heshima, yanayotambua jamii na watu walioathiriwa na mikasa kwa heshima.

## 5. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wana uwezo wa kufikia taratibu salama na bora za kushughulikia malalamishi.

**Kigezo cha Ubora:** Malalamiko hupokewa na kushughulikiwa.

**Shughuli Kuu**

**5.1** Shauriana na jamii na watu walioathiriwa kuhusu mfumo, utekelezaji na ufuatiliaji wa mchakato wa kushughulikia malalamishi.

**5.2** Pokea na ukubali malalamishi, na ushauri jinsi utaratibu unaweza kufikiwa na kiasi cha masuala unayoweza kushughulikia.

**5.3** Shughulikia malalamishi kwa wakati mwafaka, kwa njia bora na isiyo na upendeleo inayopatia kipaumbele usalama wa mlalamikaji na walioathiriwa katika hatua zote.

**Wajibu wa Shirika**

**5.4** Utaratibu wa kushughulikia malalamishi ya jamii na watu walioathiriwa na mikasa umeandikwa na upo. Utaratibu huo unafaa kujumuisha upangaji programu, dhuluma za kingono, na unyanyasaji, na matumizi mengine mabaya ya mamlaka.

**5.5** Desturi ya shirika ambapo malalamishi yanachukuliwa kwa uzito na kushughulikiwa kulingana na sera na michakato maalum ipo.

**5.6** Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanajua kikamilifu mienendo tarajiwa ya wahudumu wa usaidizi wa kibinadamu, yakiwemo maazimio ya shirika yanayohusiana na kuzuia dhuluma za kingono na unyanyasaji.

**5.7** Malalamishi yasiyoweza kushughulikiwa kwenye kiwango cha shirika yanapelekwa mahali panapofaa kwa njia inayofaa.

## 6. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapata usaidizi ulioratibiwa na wa kukamilishana.

**Kigezo cha Ubora:** Usaidizi wa kibinadamu hufanywa kwa uratibu na humarisha hali zilizopo.

**Shughuli Kuu**

**6.1** Tambua majukumu, wajibu, uwezo na mapendeleo ya washika dau tofauti.[9]

**6.2** Hakikisha usaidizi wa kibinadamu unaitangamana na ule wa kitaifa na wa mamlaka za mahali palipoathiriwa[10] na mashirika mengine ya kibinadamu.

**6.3** Shiriki katika mashirika husika ya uratibu na ushirikiane na wengine ili kupunguza mzigo kwenye jamii kutimiza kwa kiwango kikubwa utoaji huduma wa juhudi za kibinadamu.

**6.4** Shiriki habari mwafaka na wabia, makundi ya uratibu na wahusika wengine wanaofaa kupitia mbinu bora za mawasiliano.

**Wajibu wa Shirika**

**6.5** Sera na mikakati inajumuisha maazimio kwa ajili ya uratibu na ushirikiano na wengine, zikiwemo malaka za kitaifa na za mahali palipoathiriwa, bila kukiuka kanuni za kibinadamu.

**6.6** Ushirikiano na wabia hulindwa na mapatano dhahiri yanayoheshimu sehemu, majukumu na uhuru wa kila mmoja, na kutambua ugumu na maazimio ya kila mmoja.

[9] Wakiwemo wahusika wa mahali palipoathiriwa, mashirika ya kibinadamu, mamlaka za mahali palipoathiriwa, kampuni za kibinafsi na makundi mengine husika.

[10] Ambapo mamlaka ni wahusika katika mzozano huo, wahusika wa kibinadamu wanafaa kutumia dhamira yao ikilinganishwa na uhuru wa shughuli, wakizingatia mapendeleo ya jamii na watu walioathiriwa na mikasa katika maamuzi.

## 7. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanaweza kutarajia kupata usaidizi bora mashirika yanavyojifunza kutoka kwa mambo ya awali na mawazo.

**Kigezo cha Ubora:** Wasaidizi wa kibinadamu hupata maarifa na kuyaboresha kila mara.

**Shughuli Kuu**

**7.1** Zingatia mafundisho uliyopata na uliyopitia mwanzo ulipokuwa unabuni programu.

**7.2** Jifunze, vumbua na utekeleze mabidiliko kulingana na ufuatiliaji na utathmini, na maoni na malalamishi.

**7.3** Shiriki mafunzo na uvumbuzi ndani kwa ndani, na jamii na watu walioathiriwa na mikasa, na washika dau wengine.

**Wajibu wa Shirika**

**7.4** Sera za utathmini na kujifunza zipo, na kuna mbinu za kujifunza kutokana na matukio ya awali na kuboresha shughuli.

**7.5** Kuna taratibu za kurekodi ujuzi na tajiriba, na kuifanya ya kufikiwa kwenye shirika zima.

**7.6** Shirika linachangia mafunzo na uvumbuzi katika usaidizi wa kibinadamu kati ya watu sawa na katika sekta hiyo.

## 8. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanapata usaidizi wanaohitaji kutoka kwa wahudumu waajiriwa na wa kujitolea wenye ustadi na wanaosimamiwa vizuri.

**Kigezo cha Ubora:** Wahudumu[11] wanasaidiwa kufanya kazi zao ifaavyo, na wanashughulikiwa vizuri na kwa usawa.

**Shughuli Kuu**

**8.1** Wahudumu wanafanya kazi kulingana na maagizo na maadili ya shirika na kulingana na malengo na viwango vya utendakazi vilivyokubaliwa.

**8.2** Wahudumu wanazingatia sera zinazowahusu na wanaelewa matokeo ya kutozingatia sera hizo.

**8.3** Wahudumu wanajiendeleza na wanatumia ujuzi wa kibinafsi, wa kiufundi na kiusimamizi kutimiza jukumu lao na kuelewa jinsi shirika linavyoweza kuwasaidia kufanya haya.

**Wajibu wa Shirika**

**8.4** Shirika lina uwezo wa kiusimamizi na wahudumu wa kutekeleza mipango yake.

**8.5** Sera na taratibu za wahudumu ni za haki, bayana, zisizobagua na zinazofuatana na sheria ya ajira ya mahali palipoathiriwa.

**8.6** Maelezo ya kazi, malengo ya kazi na michakato ya maoni ipo hivi kwamba wahudumuwana uelewaji bayana wa matarajio.

**8.7** Kanuni ya mwenendo ipo inayoweka, kwa kiwango cha chini zaidi, jukumu la wahudumu la kutonyanyasa, kudhulumu au kubagua watu.

**8.8** Sera zipo kusaidia wahudumu kuboresha ujuzi na uwezo wao.

**8.9** Sera zipo za usalama na hali njema ya wahudumu.

[11] Wahudumu ni: mwakilishi yeyote rasmi wa shirika, wakiwemo waajiriwa wa kitaifa, kimataifa, wa kudumu au wa muda, vile vile wa kujitolea na washauri.

## 9. Jamii na watu walioathiriwa na mikasa wanaweza kutarajia kuwa mashirika yanayowasaidia yanatumia raslimali vizuri na kiuadilifu.

**Kigezo cha Ubora:** Raslimali zinasimamiwa na kutumiwa kiuadilifu kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Shughuli Kuu**

**9.1** Buni mipango na utekeleze michakato kuhakikisha utumiaji bora wa raslimali[12], kusawazisha ubora, gharama, na wakati katika kila awamu ya usaidizi.

**9.2** Dhibiti na utumie raslimali kutimiza malengo yaliyonuiwa, na kupunguza uharibifu.

**9.3** Fuatilia na kuripoti matumizi ya fedha dhidi ya bajeti.

**9.4** Unapotumia raslimali za mahali palipoathiriwa na asilia, zingatia athari kwa mazingira.

**9.5** Dhibiti hatari ya ufisadi na uchukue hatua mwafaka ufisadi unapotambulika.

**Wajibu wa Shirika**

**9.6** Sera na michakato inayosimamia utumiaji na usimamizi wa raslimali ipo, ikiwemo jinsi shirika:
a. linavyokubali na kupanga fedha na zawadi kiuadilifu na kisheria;
b. linavyotumia raslimali zake katika njia inayozingatia mazingira;
c. linavyozuia na kushughulikia ufisadi, ulaghai, mizozano na utumizi mbaya wa raslimali;
d. linavyofanya ukaguzi wa mahesabu, kuthibitisha maafikiano na kuripoti bayana;
e. linavyotathmini, kudhibiti, na kupunguza hatari kiuendelevu; na
f. linavyohakikisha kuwa kukubali raslimali hakukiuki uhuru wake.

[12] Neno “raslimali” linafaa kueleweka katika muktadha mpana, unaojumuisha ambacho shirika linahitaji ili kutimiza lengo lake, yakiwemo pamoja na mengine: fedha, wafanyakazi, bidhaa, vifaa, wakati, shamba, udongo, maji, hewa, bidhaa asilia na mazingira kwa jumla.

# viii. Faharasa

Kwa CHS, fasili hizi zitatumika:

**Uwajibikaji:** mchakato wa kutumia mamlaka vizuri, kuwajibika kwa washika dau tofauti, na kwa msingi, walio chini ya mamlaka hayo.

**Jamii na watu walioathiriwa na mikasa:** ujumla wa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana walio na mahitaji, hatari na uwezo tofauti wanaoathiriwa na mikasa, mizozo, umasikini au mikasa mingine kwenye maeneo maalum.

**Hati:** aina yoyote ya majadiliano, maafikiano, maamuzi na/au shughuli zinazoweza kupigwa chapa.

**Ustahilifu:** kiwango ambapo hatua ya kiusaidiziinaafikia malengo yake.

**Ufaafu:** kiwango ambapo matokeo ya programu za kibinadamu, stahilifu na ya kiasi, yanatimizwa kutokana na vilivyowekwa.

**Miadi:** mchakato ambapo mashirikayanawasiliana, kushauriana na/ au kukubali kushiriki kwa washika dau wanaopendelea na/ au wanaohusika, kwa kuhakikisha kuwa wasiwasi, matamanio, matarajio, mahitaji, haki na nafasi zao zinazingatiwa katika kuanzisha, kutekeleza na kukagua programu zinazowasaidia.

**Usaidizi wa kibinadamu:** shughuli inayofanywa kwa lengo la kuokoa maisha, kupunguza mateso na kudumisha heshima katika na baada ya mikasa ulioanzishwa na binadamu na mikasa asilia, vile vile shughuli ya kuzuia na kujitayarisha kwayo.[13]

**Shirika:** kitu kilicho na uongozi na mamlaka ya kutumia CHS.

**Wabia:** mashirika yanayofanya kazi kwa ushirikiano katika mpangilio rasmi kuafikia lengo maalum, yenye majukumu bayana yaliyokubaliwa.

**Sera:** hatiyoyote iliyoandikwa ya maazimio na kanuni za kufanya maamuzi.

**Kinga:** shughuli zote zinazonuia kuhakikisha uzzingatiaji kamilifu wa haki za watu pasipo kuzingatia umri, jinsia, kabila, dini, tabaka au kingine chochote. Inazidi shughuli za mara moja za kuokoa maisha ambazo huzingatiwa sana katika dharura.

**Ubora:** ujumla wa sifa bainifu za usaidizi wa kibinadamu zinazouwezesha kutosheleza mahitaji na matarajio, na kuheshimu watu wanaosaidiwa.

**Uthabiti:** uwezo wa jamii inayokumbana na hatari kukinza, kufyonza na kurejelea hali ya kawaida baada ya mikasa kwa wakati mzuri na kwa njia inayofaa.

**Wahudumu:** mwakilishi yeyote rasmi wa shirika, wakiwemo wahudumu wa kitaifa, kimataifa, na wa kudumu au wa muda, na vile vile wa kujitolea na washauri.

[13] Jinsi ilivyofasiliwa katika ALNAP Evaluation Humanitarian Action Pilot Guide, 2013, p.14.

**Kiwango Kikuu cha Kibinadamu cha Ubora na Uwajibikaji** (CHS) hutoa Maazimio Tisa ambayo mashirika na watu binafsi wanaofanya kazi katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu wanaweza kutumia kuboresha ubora na ufaafu wa usaidizi wanaotoa. CHS pia huwezesha uwajibikaji zaidi kwa jamii na watu walioathiriwa na mikasa: kufahamu maazimio ya mashirika kutawasaidia kuyashinikiza yawajibike.

Kama tarajio kuu, CHS inaeleza vipengele muhimu vya shughuli thabiti, zenye kuwajibika na bora za kibinadamu. Mashirika ya kibinadamu yanaweza kuitumia kama kanuni ya hiari ya kuendeshea taratibu zao za ndani. Pia inaweza kutumiwa kama msingi wa uthibitishaji wa utendakazi.

CHS ni tokeo la mashauriano ya miezi 12, ya awamu tatu yaliyoendeshwa na HAP International, Watu wanaotoa Misaada na Mradi wa Sphere, ambapo mamia ya watu binafsi na mashirika yalichanganua CHS na kuijaribu kwenye viwango vya makao makuu na nyanjani.

corehumanitarianstandard    @corehumstandard

www.corehumanitarianstandard.org | info@corehumanitarianstandard.org

ISBN: 978-0-9955053-1-5